(١)

# Maana halisi ya Shahada baina ya Ukweli na Madai

Imefasiriwa na

Profesa.Ayman Alasar

Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, mwenye kusema katika kitabu chake Kitukufu: {Na wala msiseme kwa yule anayeuawa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa wamekufa bali wao wako hai lakini nyinyi hamuhisi hivyo}.
Na ninashuhudia kuwa hakuna Mungu mwingine anaestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake na kwamba ninashuhudia kuwa Mtume wetu na Bwana wetu Muhammad ni Mjumbe wake. Ewe Mola wetu sala na salamu zimwendee yeye na Ali zake na Maswahaba wake na kila atakayewafuata kwa wema mpaka siku ya mwisho.

Na baada ya hayo:
Uumbaji wa Mwenyezi Mungu umekwishapitisha maamuzi kwamba yeye huwachagua katika waja wake anaewataka na kuwainua daraja na pia kulinyanyua jambo lao, na kuwamiminia mazuri yake na mema, na kuwapa ayatakayo pamoja na rehma zake, na hapana shaka kuwa cheo cha Shahada ni katika vyeo vikubwa kwa aliyowachagulia na kuwateua ambao yeye Mtukufu aliyetukuka huwapa kwa wale awatakao katika viume vyake. Ambapo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na atakayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hao watakuwa pamoja na wale aliyowaneemesha juu yao miongoni mwa Mitume, Wasema kweli, Mashahidi, na Wema, na hao ndio wenye ukaribu na waja wema zaidi}.
{Na wajue wale walioamini kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu huwachagua miongoni mwenu Mashahidi}.

Na hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu amewatengea Mashahidi mambo maalumu, na miongoni mwa hayo ni kama ifuatavyo:

Ni ule utukufu wa nafasi yako na kuwa nao karibu, na ukubwa wa malipo na neema zao . anasema Mwenyezi Mungu: {Na Mashahidi kwa Mola wao wana malipo yao na Nuru yao}.

Na kwa sababu hiyo akawakirimu kutokana na utukufu na ujirani pamoja na ukubwa wa malipo na Nuru timilifu inayotambaa katika miili yao, na anasema Masruuk Mola amrehemu:

Na nafasi hii ni Maalumu kwa Mashahidi; na hakuna kinachooonesha ukubwa wa utukufu huu kuliko Shime ya Mtume S.A.W ya kutaka kufa Shahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ili amwandikie malipo ya kiwango cha juu, anasema S.A.W: Ninaapa kwa Yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake ningependelea niuawe vitani kwa ajili ya njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kisha nihuishwe, kisha niuawe tena kisha nihuishwe, kisha niuawe tena, kutokana na ukubwa wa malipo aliyoyaandaa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa Mashahidi.

Na miongoni mwa hayo ni kwamba: Mashahidi wako hai kwa Mola wao wanaruzukiwa, wako hai katika Maisha ambayo ni tofauti na Maisha yetu, Maisha ambayo yanapindukia uwezo wa Mwanadamu kuyadiriki, nao pia wako hai katika kumbukumbu za Umma na wala hausahauliki utajo wao kwa kupita nyakati na zama mbali mbali. anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na wala msiseme kwa wale wanaouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni wafu bali wao wako hai lakini nyinyi hamuwezi kuhisi}. Na kutoka kwa Jaabir bin Adbullahi R.A anasema: Mtume S.A.W alikutana na mimi na akaniambia: Ewe Jaabir kwanini mimi ninakuona kama umenyongea? Nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, baba yangu amekufa Shahidi

Na ameacha watoto pamoja na Deni. Mtume S.A.W akasema: Je nikupe habari njema kwa yale ambayo Mwenyezi Mungu amemuandalia Baba yako? Akasema: Ndio Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Akasema: Mwenyezi Mungu hakuwahi kumsemesha mtu kamwe isipokuwa nyuma ya pazia, na amemuhuisha Baba yake na akamsemesha bila ya kizuizi – kwa maana kuwa bila ya pazia na bila ya Mtume – akasema: Ewe Mja wangu hebu tamani chochote na mimi nitakupa, akasema: Ewe Mola wangu ninatamani unihuishe ili niuawe tena kwa ajili yako, akasema Mola wake Mtukufu: Hakika mambo yalivyo uamuzi wangu umekwishatolewa kuwa wao huko hawatarejea tena. Akasema Mtume: kisha Ayah ii ikateremshwa: {Wala msiwahesabu wale ambao wameuawa katika njia ya Mwenyezi Mungu kwamba ni wafu bali wako hai kwa Mola wao wanaruzukiwa}.

Na miongoni mwayo ni: yale aliyoyasema Mtume S.A.W kuhusu utoaji wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwapa Mashahidi mambo makubwa, na vitu vizuri kwa kauli yake Mtume S.A.W aliposema: Shahidi ana mambo sita kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu: anamsamehe kwa tone la kwanza la damu yake, na anaoneshwa kiti chake peponi, na anaepushwa na adhabu ya kaburini, na anasalimika na mfadhaiko mkubwa, na anavalishwa nguo ya Imani, na anaozeshwa Hurul-aini, na anapewa nafasi ya kuwaombea Shifaa ndugu zake sabini. Na kauli yake Mtume S.A.W aliposema: Na ninaapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake, hakuna yoyote atakayesemeshwa katika njia ya Mwenyezi Mungu – ninaapa kwa Mwenyezi Mungu atakayemsemeshwa katika njia ya Mwenyezi Mungu – isipokuwa atakuja siku ya Kiama akiwa na rangi ambayo ni Rangi ya Damu na harufu Harufu ya Miski.

Ni kwamba sisi tunasisitiza kuwa nafasi hii ni ya hali ya juu mno

Na ni daaraja la juu aliloliandaa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa Mashahidi ambalo hawezi kulipata daraja hili isipokuwa Shahidi wa kweli, kwani kuna Shahidi wa kweli na kuna mtu aliyeuawa kwa makosa. Shahidi ni yule aliyeipigania nchi yake dhidi ya kila aina ya adui, na akajitoa muhanga kwa ajili hiyo, na kuulinda mchanga wa nchi yake na kwa ajili ya kuwalinda watu wake na kila anayeishi katika ardhi hiyo, akifanya hivyo kwa kutaka radhi za Mola wake Mtukufu. Kwani Nchi na Heshima hatari yake sio ndogo na Nafasi yake pia kuliko nafsi, Dini na Mali, hiyo ni katika Makusudio Makuu ambayo Sheria Tukufu ya Uislamu imesisitizia umuhimu wa kuyalinda. Mtume S.A.W amesema: Mtu yoyote atakayeuawa kwa ajili ya kuilinda Mali yake basi yeye ni Shahidi, na atakayeuawa kwa ajili ya Watu wake, au Uhai wake au Dini yake basi Mtu huyo ni Shahidi. Na kuna Mtu mmoja alimjia Mtume S.A.W akamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu je unaonaje akija mtu anataka kuichukua mali yangu nifanyeje? Mtume S.A.W akasema: Na usimpe Mali yako. Akasema: Na je unaonaje ikiwa atapigana na mimi? Mtume akasema: Upigane nae. Akasema: Na je unaonaje ikiwa ataniua mimi? Mtume akasema: Wewe utakuwa Shahidi. Akasema: Je unaonaje ikiwa mimi nitamuua? Mtume S.A.W akasema: Yeye atakuwa ni mtu wa Motoni.

Ama kuhusu mtu aliyeuawa kwa ajili ya batili ni yule ambaye anawaua watu wasio kuwa na hatia yoyote, na anawatisha wananchi, na anatishia usalama na amani yao na anatumi uwezo wake kueneza ufisadi na machafuko duniani na anawatishia usalama watu walio na utulivu kwa kutumia vitendo vya kujilipua, na milipuko ya kigaidi haikubaliki katika Dini ya Uislamu na wala haikubaliki kiakili na wala anayejiua hazingatiwi kuwa ni Shahidi

Na kumpa wasifu wa Shahidi ni madai ya uongo yasiyosihi, na kwa kulibadilisha neno kwa kulitoa katika sehemu yake.

Taarifa ya Al-Azhar Al-Sharif katika Misri iliyotolewa tarehe 23-2-2019, imesisitiza juu ya kuyaangamiza baadhi ya madai ya Makundi

ya Kigaidi ya kwamba Mashahidi wa Kweli ni wale wanaozilinda nchi zao dhidi ya kila aina ya adui na wanajitolea muhanga Roho zao kwa ajili ya kuilinda nchi yao, na anga lake, na watu wake na kila anayeishi humo. Na wala sio hawa ambao wanawatisha watu katika nchi zao na wanautishia usalama na amani yao na wanafanya juhudi za kueneza ufisadi na machafuko katika maeneo mbali mbali ya nchi hiyo.

Na wala haogopi kuwa miongoni mwa wajibu wa Mwislamu ni kuwa mtekelezaji wa wa ahadi na anaipenda nchi yake, na anaikinga na kuilinda na maadui kwa nguvu zote alizo nazo kwa kauli au vitendo, na kwamba kuipenda nchi ni sehemu ya Imani na kwamba hilo ni katika mambo yanayoungwa mkono na Akida ya Uislamu na Sunna ya Mtume S.A.W, bali waungwana wanakubaliana hivyo pamoja na wenye akili zilizonyooka.

Na Ofisi ya Fatwa Ya Misri imetoa Fatwa nyingi ambazo zinayaelezea masuala kama haya ya kigaidi, na kwamba kuyafanya kwa njia yoyote miongoni mwa njia ya kujitoa muhanga ambayo inazingatiwa kuwa ni katika Madhambi makubwa mno mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwani mtu yoyote anayefanya hivyo ni mjinga anayeitumbukiza nafsi yake katika umauti kwa kuuvamia, na Mkweli Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: {Na wala msiziue nafsi zenu}. Na Mtume wetu S.A.W anasema: Mtu yoyote atakayejiua yeye mwenyewe kwa chuma basi chuma hicho mkononi mwake kitatiwa tumboni mwake ndani ya Jahanna na atakaa humo milele na milele. Na Imamu Nawawiy aliiwekea Hadithi hii mlango katika Ushereheshaji wake wa Sahiihu Muslim akasema: "Mlango wa Uzito wa kuharamisha mtu mujiua yeye mwenyewe"

Na kwamba mtu yoyote atakayejiua yeye mwenyewe kwa kitu chochte ataadhibiwa kwacho motoni". Na Hadithi hii na mfano wake, inathibitisha kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema: {JE yule mwenye kupambiwa matendo yake maovu na kayaona kuwa mazuri…}

Ni kwamba sisi tunafafanua kuwa mtu yoyote anayefanya vitendo hivi vya kigaidi vya kujiua ni mfuasi wa fikra za Madhehebu yenye msimamo mkali yatokanayo na Khawaarij na wale waliokuja baada ya Khawaarij miongoni mwa makundi yaliyopotea na yanayowapoteza watu wengine ambayo yanaikufurisha Jamii na kuhalalisha Mauaji yao.

Hakika mambo yalivyo, njia za milipuko, uangamizaji, uharibifu, mauaji ya kisiasa, na kujiua ni katika mambo yaliyoharamishwa Kisheria na hakuna hitilafu katika hayo, ambapo yote hayo anaenda kinyume na maandiko ya Sheria tukufu inayoamrisha uwajibu wa kulinda Nafsi, Nchi na Mali, na mtu kujipeleka katika maangamizi yeye mwenyewe na kuitoa roho yake au kuzishambulia roho za watu wengine, na kufanya uharibifu ardhini, vyote hivyo ni katika yaliyoharamishwa na Sheria tukufu.

Uislamu umesisitiza kwa msisitizo mkubwa juu ya Uharamu wa kumwaga damu za watu na ulazima wa kuzilinda. Mtume wetu S.A.W aliianza hotuba yake ya kusanyifu katika Hijja ya kuaga kwa kauli yake S.A.W: Hakika Damu yenu na Mali zenu na Heshima zenu ni haramu kwenu (kuvunjwa), kama ilivyo na Uharamu wa Siku yenu hii, katika nchi yenu hii na katika mwezi wenu huu, na mtakutana na Mola wenu na atakuulizeni kuhusu matendo yenu kwa hiyo msirejee baada yangu katika ukafiri – au upotofu – mkapigana nyinyi wenyewe kwa wenyewe, kisha Mtume S.A.W, akasema: Mja anaendelea kuwa katika nafasi katika dini yake ikiwa hajapatwa na Damu ya Haramu. Na kutoka kwa Abdullahi bin Omar R.A, amesema: Nilimwona Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W, akitufu Kaabah huku akisema: Uzuri wako ulioje, na uzuri wa harufu yako, na utkufu wako ulioje, na Heshima yako iliyoje, na ninaapa kwa yule ambaye Nafsi ya Muhammad iko mikononi mwake, hakika utukufu wa Muumini ni

mkubwa zaidi ya Utukufu wako, Mali yake na Damu yake, na tumdhanie isipokuwa kheri tupu.

Na Uislamu umekataza kumuua mtu ambaye Mwenyezi Mungu amehamisha kuuawa kwake isipokuwa kwa Haki na ukapangilia suala hili kwa ahadi ya adhabu kali mno ambapo Mwenyezi Mungu anasema: {Na yoyote atakayemuua muumini kwa makusudi basi malipo yake ni Jahannamu, ataishi humo milele, na Mwenyezi Mungu atakuwa amemkasirikia na amemlaani na amemwandalia adhabu kali mno}.

Ninayasema maneno yangu haya na ninajiombea na kukuombeeni kwa Mwenyezi Mungu msamaha

* * *

Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu, na rehma na amani ziwe juu ya Mtume wetu Muhammad, na Ali zake na Maswahaba wake na yoyote atakayewafuata kwa wema mpaka siku ya Malipo.

Ndugu zangu Waislamu.

Hakika kuyafikia Malengo Makubwa na kupata matokeo makubwa katika maisha haya kuna hitaji kujitolea yale yanayoendana na sifa ya Malengo na utukufu wa Makusudio na kuyafikia matokeo yake, na katika kujitolea kunakokuja nafasi ya juu ni kujitlea nafsi na kujitoa kwa ajili ya njia ya Mwenyezi Mungu kwa kuilinda nchi, utukufu wake na heshima yake.

Na sisi tunahuisha Makaribisho ya Siku ya Mashahidi, hakika sisi tunajikumbusha kuhusu hawa ndugu zetu ambao Roho zao imepevuka kwa daraja na kwenda kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na wakazipata radhi zake, ambao ni katika wanajeshi wetu wa jeshi la

ulinzi na jeshi la polisi pamoja na wananchi walio na nia safi katika mstari wa mbele wa mapambano dhidi ya ugaidi, hsari na giza.

Hawa Mashujaa ndio haswa Mashahidi wa kweli, na kuna toauti kubwa baina ya ukweli na madai, kwani hawa Mashujaa ni ndugu zetu

Kwani hawa Mashujaa ndio waliouhuisha ndani yetu moyo wa Utukufu na Maadili mea, Majigambo na Heshima yetu, na wakafanikiwa kuilinda Misri na nafasi yake pamoja na heba yake, na bado walinzi wa nchi wanafanya juhudi kubwa ya kujitolea nafsi zao katika njia ya kupambana na Ugaidi Mwovu na makundi mengine yanayowakufurisha watu yaliyopotea na yanayopotosha. Na sisi tuna yakini na imani ya nusra ya Mwenyezi Mungu kwao.

Na hakika sisi tunatarajia kwa nafsi zetu kupata Shahada katika njia ya Mwenyezi Mungu na kwa ajili ya Taifa, na kwa nini isiwe hivyo? Wakati Mtume S.A.W amesema: Mtu yoyote atakayemwomba Mwenyezi Mungu Shahada kwa imani ya kweli, basi Mwenyezi Mungu atamfikisha katika ngazi za Mashahidi hata kama Mtu huyu atafia kitandani kwake.

Hakika wajibu wetu katika kipindi hichi ambacho nchi zitu inakipitia tunatakiwa kufanya juhudi ya kuzilinda na kumzuia adui yoyote au hatari yoyote inayotishia usalama na utulivu wake, na kufanya kazi kwa kila tulichojaaliwa miongoni mwa nguvu katika kuendeleza mwendo wa ujenzi na uendelezaji wa miji, kwani Dini yetu ina ufundi wa kutengeneza maisha na wala sio kutengeneza vifo, na Dini ya Ujenzi na Uendelezaji sio ya Ufisadi na uharibifu. Na ni jukumu letu kuwa bega kwa bega kwa ajili ya kumzuia kila mwenye kutaka kuzivuruga nchi zetu na ambaye anapanga mikakati ya kila aina, na lengo lake ni kuiangusha Nchi yetu, Ardhi yake na watu

wake. Wanaseimama mbele ya Nchi yetu, watu wenye kujitolea miongoni mwa wananchi wa Nchi yetu na kuzitoa muhanga roho zao na damu zao na mali zao kwa ajili ya kuilinda nchi na kuzilinda ardhi zake zote. Kwani Nchi yetu ni miongoni mwa ngao ya nchi nyingine za Moyo hai wa Uislamu. Na kuilinda nchi ni wajibu wa Kisheria na ni haki ya kidini, na kuiangusha Misri ni kuuangusha Uislamu na kuwatia unyonge Waislamu wa nchi zote, na kwa hivyo, tunatakiwa sote tusimame kidete tukiwa wamoja kwa ajili ya kuilinda nchi kutokana na ufisadi wa mafisadi na ujanja ujanja pamoja na chuki za wenye nazo.

Ewe Mola wetu turuzuku Shahada katika njia yako
Na utujaalie tuwe miongoni mwa waja wako wachamungu, na uzilinde nchi zetu na kila ubaya na uovu